AZIMIO NO. 202122-1
USALAMA NA KUWAKARIBISHA SHULENI

AMBAPO bodi ya wakurugenzi wa shule za Umma za Salem-Keizer waliochaguliwa na watu kutoa uongozi na maono kwa shule za Umma za Salem-Keizer kwa kutunga na kukuza elimu itayokayoleta manufaa kwa maisha ya wanafunzi wote K-12; na

AMBAPO Shule za Umma za Salem-Keizer imejidhatiti kutoa mazingira na nafasi salama yenye ukaribisho ambapo wanafunzi wote wataweza kuweka mkazo kwenye elimu na kupata ujuzi wa maarifa na wilaya itatoa msaada wa usalama na ustadi wakati ikitoa nafasi ya fursa na kupata elimu yenye kiwango cha juu; na

AMBAPO kujidhatiti huku haimaanishi kuwa mafanikio ya mwanafunzi yatatabiriwa au kuamuliwa na rangi, asili ya utaifa, dini, uasilia na mavazi ya kidini, uwezo, hali ya kiuchumi, uhamaji, lugha ya asili, kijinsia, aina ya uhamiaji, utambuzi wa kijinsia au kiwango cha ustadi wakati anaanza shule; na

AMBAPO bodi ya shule imejidhatiti kulinda haki ya katiba kwa wanafunzi, kujumuisha haki ya nne ya katiba ya kuwa huru kutokana na misako na mashambulio yasiyofaa na kuweza kupata elimu ya bure ya umma; na

AMBAPO bodi ya shule inaamini kuwa shughuli ya utekelezaji wa sheria za uhamiaji na vyombo vya sheria kwenye shule za Umma za Salem-Keizer kwenye njia za usafiri, kwenye mali za wilaya na/au wakati wa shughuli za shule zitachangia kuingilia uwezo wa wilaya kutoa mazingira salama na sehemu ya ukaribisho kwa kuingiliana na haki ya mwanafunzi wa Salem-Keizer; na

AMBAPO bodi ya shule haitavumilia aina yeyote ile ya ubagauzi, hotuba za chuki, matamshi ya kibaguzi, pamoja na ubaguzi kuhusu uasilia na mavazi ya kidini, kushurutishwa, unyanyasaji, vitisho, uonevu, unyanyasaji wa kwenye mtandao au kutishia wanafunzi; watoto wanaoshuhudia vurugu au mateso wanaweza wasijikie salama au wasiwe tayari kusoma; na hawa watoto waliodhurika wanaweza kuathiri wanafunzi wenzao, watu wazima na wilaya na jamii ya shule ambayo inaingiliana nao; na

AMBAPO bodi ya shule imetambua kuwa matukio ya kitaifa na hali iliyopo sasa ya kisiasa imesababisha kuleta wasiwasi na hofu kwa jamii kubwa na tunajukumu la kushirikiana katika kuangalia hii hali kwa niaba ya watalaamu wa elimu wa shule za Umma za Salem-Keizer, wanafunzi na familia kukuza uponyaji, maelewano na upatanisho kwa jamii yetu.

SASA BASI IWE IMETATULIWA bodi ya shule inategemea wilaya kufanya kila kitu kwa kutumia mamlaka yake kulinda taarifa za siri za wanafunzi wa Salem-Keizer na kuhakikishia kuwa mazingira yao ya kusoma hayaingiliwi na vitendo vya utekelezaji vya uhamiaji kujumuisha, lakini siyo haya tu, yafuatayo:

Wilaya itaendelea kutokuuliza, kukusanya au kulinda taarifa kuhusu wanafunzi wa Salem-Keizer au familia zao kuhusiana hali ya yao ya uhamiaji.

Maombi yeyeto ya afisa uhamiaji (a) kuingia kwenye shule za wilaya au maeneo ya wilaya (b) kuwasiliana na mwanafunzi yeyote wakati mwanafunzi akiwa chini ya usimamizi wa wilaya wakati wowote wa shughuli za shule au wakati anapotumia usafiri au (c) kwa taarifa yeyeto kuhusu mwanafunzi wa Salem-Keizer inatakiwa kupelekwa ofisi ya mshauri wa sheria. Kujibu hilo ombi,

mshauri wa sheria wa wilaya hata toa taarifa au kuwapatia taarifa za mwanafunzi wa Salem-Keizer isipokuwa pale watakapowakilisha hati halali ya kukamatwa iliyotolewa na jaji wa shirikisho au serikali au hakimu.

IWE IMESULUHISHWA ZAIDI wilaya itatoa mafunzo na nyenzo za ziada kama zitahitajika kwa migogoro iliyopo na tahadhari ya kukabiliana na dharura ili kuhakikisha na kusaidia usalama na ustawi kwa wanafunzi wa Salem-Keizer ambao watakuwa wameathirika na hatua za utekezaji wa uhamiaji; na

IWE IMESULUHISWA ZAIDI wafanyakazi wote wa wilaya watafanya bidii kutambua na kuelezea unyanyasaji, ubaguzi wa rangi, kushurutishwa, unyanyasaji, vitisho, kunyanyaswa, kunyanyaswa kwenye mtandao au kutishwa kwa sera ya uongozi (Instruction - A003); wafanyakazi wataarifiwa na kufuata sera (Instruction - A035) inayohusiana na kushughulikia utekelezaji wa sheria isiyo ya ndani, ikiwa ni pamoja na maafisa wa uhamiaji wanaoingia kwenye maeneo ya wilaya, na sera ya utalawa na utaratibu kuhusiana na kushughulikia malalamiko (Administrative-ADOS na P008); na

Wafanyakazi wote wa wilaya watadumisha utamaduni wa shirika kwa kuonyesha wanafunzi na familia zao nidhamu, utu na adabu na kujitahidi kutengeneza na kukuza mazingira shirikishi na ya kukaribisha wanafunzi wote na familia; na

Superintendent atazingatia, kuendeleza, mawasiliano na kutekeleza sera za utawala na utaratibu utakaoweka mazingira salama, shirikishi na ya kukaribisha na kufurahia utajiri wa watu mbalimbali na imani inayopatikana ndani ya jamii ya Salem-Keizer

Superintendent atachukua hatua mahususi kuzuia na/kurekebisha hali sahihi, taratibu, hatua au uamuzi ambao ni kinyume na sheria, unyoofu, siyo usalama, siyo ya maadali, hayana nidhamu, yenye vurugu au inayokiuka bodi au sera za utawala; na

Bodi ya shule imejidhatiti kutambua na kurekebisha mazoea na sera zinazosababisha na kuchangia fursa za nafasi, pengo la maendeleo na ubaguzi wa rangi katika maeneo yote ya wilaya na bodi ya shule. Bodi ya shule inatambua maumivu yaliyosababishwa na mfumo wa ubaguzi na matendo ya ubaguzi. Bodi ya shule imejidhatiti kuelewa kuhusu maumivu yaliyosababishwa na ubaguzi wa rangi, njia za kuondoa aina zote za ubaguzi wa rangi na kuelewa kuhusu upendeleo wenyewe. Bodi ya shule imeendelea mbele zaidi na kukuza usawa ili kuhusisha mazingira ya kuwa kila mwanafunzi, mfanyakazi, familia na watu kwenye jamii.

IWE IMESULUHISWA ZAIDI ya kuwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shule za Umma za Salem-Keizer imejidhatiti kikamilifu kwa hili azimio na tutalipitia, kurudia kama itahitajika na kulithibitisha azimio hili kila mwak.

_____ 9/14/21

Osvaldo F. Avila, Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi Tarehe
Shule za Umma za Salem-Keizer